

**HOTUBA YA WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO,
MHESHIMIWA NAPE MOSES NNAUYE KWENYE TAFRIJA FUPI (COCKTAIL
PARTY) ILIYOANDALIWA NA KAMPUNI YA MWANANCHI
COMMUNICATIONS LIMITED KWA AJILI YA BODI YA MWANANCHI,
WATEJA WAKE NA WADAU WA HABARI TAREHE 02/03/2016**

Mwenyekiti Mtendaji wa Makampuni ya National Media Group, Bw Wilfred Kiboro.

Mwenyekiti wa Bodi ya Mwananchi Communications Limited Tanzania, Bw. Leonard Mususa.

Katibu Mkuu Wizara ya Habari, utamaduni, sanaa na Michezo, Prof. Elisante Ole Gabriel.

Mkurugenzi Mkuu Idara ya Habari (Maelezo) Bw. Assah Mwambene.

Mkurugenzi Mkuu National Media Group, Bw. Joe Muganda.

Mkurugenzi Mkuu Mwananchi Communications Limited, Bw. Francis Nanai

Wageni waalikwa,

Waandishi wa Habari

Mabibi na mabwana,

Itifaki imezingatiwa,

Awali ya yote napenda kumshukuru mwenyezi mungu mwingi wa rehema kwa kutukutanisha sote hapa jioni hii ya leo.

Nikiwa kama mshirika muhimu na Waziri mwenye dhamana katika sekta hii ya habari hapa nchini, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru sana vyombo vya habari kwa kuwahabarisha watanzania katika mchakato wote wa uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 na pia katika siku mia za kwanza za Raisi wa awamu ya 5, Mheshimiwa Dr. John Joseph Pombe Magufuli. Hakika mmeonyesha uwezo mkubwa, weledi na ukomavu katika uandishi wa habari.

Pili, serikali yetu ya awamu ya 5 ina dhamira ya dhati kabisa ya kushirikiana na wadau wote hasa katika sekta binafsi, hivyo basi wizara yangu inakusudia kushirikiana vyema na vyombo vyote vya habari na kuangalia upya sheria ya vyombo vya habari ya mwaka 1976 ya huduma za vyombo vya habari. Tutaifanyia kazi kwa kushirikiana pamoja na nyinyi wadau wetu wa habari kabla ya kuzirudisha tena bungeni

Mabibi na Mabwana,

Kama ilivyo katika nchi yeyote upashanaji habari ni muhimu sana kwa taifa letu hivyo basi wizara yangu imejipanga vyema kufanya kazi na vyombo vyote vya habari kwa ukaribu zaidi bila kuangalia ni cha serikali chama au sekta binafsi.

Napenda pia kuchukua fursa hii kuupongeza uongozi mpya wa Jukwaa la Wahariri Tanzania na napenda kuwahakikishia kwamba tutafanya kazi pamoja na kwa ushirikiano wa hali ya juu.

Tukiwa tunashuhudia kupiga hatua kwa kiasi kikubwa katika shughuli za kila siku na hasa katika sekta hii ya habari, napenda kuwaasa nyie wanahabari kuandika habari za uhakika bila kuchochea upande wowote maana nchi yetu ni yenye amani na tungependa amani na upendo tuliokuwa nao watanzania ubakie hivyo hivyo na tubakie kioo cha amani Afrika ya Mashariki, Afrika na Duniani kwa ujumla.

Pili serikali itaendelea kufanya biashara na vyombo vyote vya habari hasa upande wa matangazo.

Mabibi na Mabwana,

Mwisho napenda kuwashukuru uongozi wote wa Nation Media group na Mwananchi Communications Limited kwa kunialika leo niwe mgeni rasmi na nawashukuru wageni wote kwa kufika hapa jioni hii ya leo. Napenda pia kuwapongeza kwa hafla nzuri mliyoandaa jioni hii ya leo na mwisho kabisa nashukuru sana kwa kunisikiliza. Ni matumaini yangu kuwa tukio hili litakuwa chachu ya mambo mengi mazuri kwa biashara yenu.

Asanteni sana.